# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 11 YA MWAKA 2004 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.
2. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR

3. Uanzishwaji wa Mamlaka.
4. Madhumuni na malengo ya Mamlaka.
5. Kazi za Mamlaka.
6. Uwezo wa Mamlaka.
7. Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji.

### SEHEMU YA TATU
### USIMAMIZI WA MAMLAKA

8. Uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi.
9. Muda wa wajumbe.
10. Akidi.
11. Utaratibu wa vikao.
12. Vikao vya Bodi.
13. Maamuzi.

14. Posho la wajumbe.

15. Mjumbe mualikwa.

16. Ukomo wa wajumbe.

17. Uwezo na kazi za Bodi.

18. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

19. Watendaji wa Mamlaka.

**SEHEMU YA NNE**
**HAKI, WAJIBU NA MAKATAZO KWA WAWEKEZAJI**

20. Haki ya mwekezaji.

21. Wajibu wa Mwekezaji Aliyeidhinishwa.

22. Katazo.

**SEHEMU YA TANO**
**UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI KWA MIRADI ILIYOIDHINISHWA**

23. Maombi ya Cheti cha Uwekezaji.

24. Yanayotakiwa kuwemo katika Cheti cha Uwekezaji.

25. Kusitisha na kufuta Cheti cha Uwekezaji.

26. Athari za kufutwa kwa Cheti.

27. Marekebisho ya cheti.

**SEHEMU YA SITA**
**FURSA NA VIVUTIO VYA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA**

28. Upatikanaji wa leseni, vibali na huduma nyengine.

29. Ajira kwa wataalamu wageni.

30. Upatikanaji wa ardhi.

31. Vivutio na ruhusa.

## SEHEMU YA SABA
## DHAMANA KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA


32. Haki ya kuhaulisha fedha.

33. Kinga dhidi ya kuchukuliwa mali kwa lazima.

34. Utatuzi wa migogoro.


## SEHEMU YA NANE
## MAENEO HURU YA UCHUMI


35. Utambuzi na utangazaji wa Maeneo Huru ya Uchumi.

36. Malengo na madhumuni.

37. Kutambuliwa bidhaa kuwa imeingizwa au imesafirishwa nje ya nchi.

38. Bidhaa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi.

39. Uhamishaji wa bidhaa kutoka Maeneo Huru ya Uchumi.

40. Eneo la Forodha.


## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI YA FEDHA


41. Fedha za Mamlaka.

42. Bajeti ya mwaka.

43. Hesabu na ukaguzi.


## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI MENGINEYO


44. Utunzaji siri.

45. Rufaa.

46. Mradi uliotelekezwa.

47. Makosa na adhabu.

48. Kanuni.

49. Kufuta na kubakiza.

JADWELI

**SHERIA NAM. 14 YA 2018**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

31 Disemba, 2018

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 11 YA MWAKA 2004 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, 2018 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Eneo la Kilimo" maana yake ni eneo huru la kiuchumi lililotangazwa chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii kwa kuimarisha sekta ya kilimo, huduma zake na shughuli zinazohusiana nazo;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"Iliyoidhinishwa" kuhusiana na uwekezaji fedha za kigeni, muda, mafao, vivutio, kiwango au idadi maana yake ni biashara yoyote, fedha, muda, mafao vivutio, kiwango au idadi iliyoelezwa katika nyaraka husika iliyotolewa na Mamlaka;

"Mradi Ulioidhinishwa wa Mgeni" maana yake ni uwekezaji uliowekezwa Zanzibar ambao kiwango cha zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zake zinamilikiwa na mgeni;

"Mradi Ulioidhinishwa wa Mwenyeji" maana yake ni uwekezaji uliowekezwa Zanzibar ambao kiwango cha zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zake kinamilikwa na Mtanzania;

"Mwekezaji Aliyeidhinishwa" maana yake ni mwekezaji mgeni aliyeidhinishwa au mwekezaji mzawa aliyeidhinishwa na ambae cheti chake cha uwekezaji kimetolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8(1) cha Sheria hii;

"Kibali cha Ujenzi" maana yake ni kibali kinachotolewa na Kitengo cha Kudhibiti Ujenzi kwa lengo la ujenzi wa Mradi ulioidhinishwa;

"Eneo la huduma za biashara" maana yake ni Eneo Huru la Kiuchumi lililotangazwa chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii ili kuwezesha utoaji wa huduma zikijumuisha pamoja na Makao makuu ya biashara ya kikanda, vituo vya majadiliano ya kibiashara, vituo vya simu vya kimataifa, vituo vya biashara za hisa, huduma za ushauri, uendeshaji wa biashara pamoja na huduma nyengine zinazohusiana;

"Mtaji" maana yake ni michango yote ya fedha taslim, kiwanda, mitambo, zana, majengo, vipuri na mali yoyote ya kibiashara inayoweza kudumu zaidi ya miezi kumi na mbili isipokuwa thamani ya bidhaa ya biashara ambayo haitumiki katika shughuli za kawaida za biashara;

"Cheti cha uwekezaji" inajumuisha leseni, ruhusa na kibali chochote kinachoruhusu uanzishwaji wa biashara ambayo itamfanya mwekezaji awajibike kukipata kwa mujibu wa Sheria hii;

"Muda wa ujenzi" maana yake ni muda ulioruhusiwa na Mamlaka kwa Mwekezaji kukamilisha ujenzi kwa mujibu wa kibali cha ujenzi kilichotolewa na Kitengo cha Kudhibiti Ujenzi;

"Awamu ya ujenzi" maana yake ni muda ulioruhusiwa na Mamlaka kwa ajili ya kujenga sehemu ya mradi kwa mujibu wa mpango wa uwekezaji ambao umewasilishwa na Mwekezaji na kuidhinishwa na Mamlaka;

"Udhibiti wa Forodha" maana yake ni utaratibu uliowekwa kuhakikisha kwamba Kanuni chini ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 zinatekelezwa;

"Eneo la Udhibiti wa Forodha" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi ambalo baadhi ya wawekezaji wanafanya biashara zenye udhibiti wa forodha;

"Mipaka ya forodha" maana yake ni mipaka ya kijografia katika Jamhuri ya Muungano Tanzania na nchi nyengine yoyote iliyopewa uanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya Ibara ya 3 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini haijumuishi maeneo huru ya kiuchumi;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni mtu alieteuliwa chini ya kifungu cha 18(1) cha Sheria hii na inajumuisha afisa yoyote aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu kwa niaba yake pale ambapo itawezekana;

"Usafirishaji wa nje" maana yake ni kuchukua au kusababisha kuchukua bidhaa nje ya mipaka ya forodha au eneo huru la uchumi;

"Mwendelezaji" maana yake ni Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae anajihusisha au amepanga kuendeleza na ambae ataendesha au kutokuendesha au amepanga kuendesha eneo la ukanda huru wa uchumi kwa mujibu wa Sheria hii;

"Eneo la uvuvi" maana yake ni eneo huru la uchumi lililotengwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii ili kuimarisha sekta ya uvuvi, huduma zake na shughuli zinazohusiana nazo;

"Mali za kigeni" inajumuisha fedha ya kigeni inayobadilishika bila ya kikwazo na fedha nyengine yoyote, mitaji, haki, mafao au mali, ikiwa halisi au sio halisi iliyopatikana kwa matumizi ya fedha za kigeni na marejesho yake yametokana katika mitaji, haki, mafao au mali;

"Raia wa kigeni" maana yake ni:

(a) mtu asiyekuwa Mtanzania; au

(b) Kampuni ambayo:

(i) imesajiliwa nje ya Zanzibar; au

(ii) imesajiliwa ndani ya Zanzibar lakini ni kampuni ambayo Mamlaka imejiridhisha kuwa hisa yake zaidi ya asilimia hamsini zinamilikiwa na raia wa kigeni.

"Mwendeshaji" maana yake ni Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae anajihusisha na usimamizi au uendeshaji wa Eneo Huru la Uchumi na ambae amethibishwa kwa kazi hiyo kwa mujibu wa Sheria hii;

"Maeneo huru ya uchumi" maana yake ni eneo lililotangazwa kwa shughuli hiyo chini ya kifungu 35 cha Sheria hii na ambalo linajumuisha eneo la viwanda la Amani, eneo la Fumba, eneo la Micheweni, eneo la Uwanja wa ndege, eneo la Maruhubi au eneo jengine lolote litakalotangazwa na Rais kwa shughuli hiyo;

"Maeneo ya Bandari Huru" maana yake ni eneo lililotangazwa ambalo lipo katika Eneo Huru la Uchumi ambapo bidhaa zilizoingizwa katika eneo hilo kiujumla zinachukuliwa, kama ushuru wa uingizaji umezingatiwa, ambazo zipo nje ya mipaka ya forodha na inajumuisha Eneo Huru la Bandari la Maruhubi, Eneo Huru la Bandari la Uwanja wa Ndege au eneo lolote ambalo litatangazwa kama eneo la Bandari Huru na Rais;

"Eneo Huru la Biashara" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi linalodhibitiwa na Eneo la Forodha ambapo bidhaa hushushwa kwa ajili ya kusafirishwa, kuhifadhiwa na inaweza kujumuisha kupunguzwa na kufunganishwa upya, kupembua, kuchanganya, kuuza au aina nyengine ya uhifadhi ukiondoa uzalishaji na uchakataji;

"Maeneo yaliyopungukiwa na fursa za kiuchumi" maana yake ni maeneo ya uwekezaji yaliyopungukiwa na fursa za kiuchumi na inaweza kujumuisha ukosefu wa miundombinu ya msingi;

"Bidhaa" inajumuisha aina zote za bidhaa, wanyama, mizigo, maghala, malighafi, fedha na inajumuisha bidhaa za posta isipokuwa mawasiliano binafsi na endapo bidhaa hizo zitauzwa chini ya Sheria hii, mapato yatokanayo na bidhaa hizo;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

"Uingizaji" maana yake ni kuingiza au kusababisha kuingizwa katika mipaka ya Forodha au Maeneo Huru ya Uchumi;

"Ushuru wa uingizaji" maana yake ni aina yoyote ya ushuru wa forodha na tozo nyengine yenye athari inayofanana ambayo inatozwa katika bidhaa iliyoingizwa;

"Eneo la viwanda" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi lililotengwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii, ambalo litakuwa na miundombinu wezeshi ili kurahisisha mahitaji ya viwanda vya uzalishaji na uchakataji;

"Eneo la teknolojia ya habari na mawasiliano" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi lililotengwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii ili kuimarisha sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano, huduma zake na shughuli zinazohusiana nazo;

"Miundombinu" maana yake ni barabara, nishati, maji, michirizi, mawasiliano, huduma za usafi au mitambo ya usafishaji maji, mitandao, majengo au huduma nyengine ambazo ni muhimu kwa uendelezaji na utekelezaji wa miradi iliyoidhishwa na muafaka kwa sekta husika au kwa mtazamo wa kundi maalum;

"Mwekezaji" maana yake ni mtu au Kampuni yenye kujitegemea ambayo ipo katika hatua za kuwekeza, anawekeza au tayari ameshawekeza kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Uwekezaji" inajumuisha mchango wa mtaji wa ndani au nje uliotolewa na wawekezaji au kampuni pamoja na kuanzisha au kununua mali za kibiashara kunakofanywa na, au kwa ajili ya mradi wa biashara na utajumuisha utanuzi, marekebisho, kuimarisha au kukarabati mradi wa biashara;

"Cheti cha Uwekezaji" maana yake ni cheti kinachotolewa chini ya masharti ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii;

"Eneo la Mifugo" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi lililotengwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii, ambalo shughuli zifuatazo zinafanywa; ukaguzi wa wanyama, kulisha wanyama, kunenepesha, machinjio na uhifadhi, kuondoa mifupa, kuongeza thamani, uzalishaji dawa za mifugo na shughuli nyengine zinazohusiana nazo;

"Ardhi" maana yake ni ardhi kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Umiliki wa Ardhi;

"Utengenezaji" maana yake ni kutengeneza, kuzalisha, kuunganisha, kuchakata au kuzalisha kwa mkono, kiufundi, kikemikali au kibayokemia kunakojumuisha uchakataji kama vile, uhifadhi, ukataji, ung'arishaji, usagishaji, usarifu wa madini na utengenezaji upya ili kupata bidhaa mpya yenye jina, tabia na matumizi tofauti;

"Waziri" maana yake ni waziri anayehusika na masuala ya uwekezaji;

"Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji" maana yake ni mfumo unaosaidia na unarahisisha uwekezaji ambao huwaweka pamoja watendaji wa taasisi za Serikali zinazotoa huduma kwa wawekezaji katika Mamlaka kwa lengo la kutoa huduma za kiufanisi na kwa uwazi kwa wawekezaji;

"Hisa za Upendeleo" maana yake ni hisa ambazo mmiliki wake hupata gawio ambalo halibadiliki, malipo yake yanapewa kipaumbele kuliko katika mgawanyo wa hisa za kawaida;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Ofisa Stahiki" maana yake ni ofisa aliyeruhusiwa na Mamlaka ya forodha kusimamia masuala ya forodha katika Maeneo Huru ya Uchumi;

"Eneo la Sayansi na Teknolojia" maana yake ni Eneo Huru la Uchumi lililotengwa kwa madhumuni hayo chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii ili kuimarisha sekta ya sayansi na teknolojia na huduma zake na shughuli zinazohusiana nazo;

"Uwekezaji Mkakati" maana yake ni uwekezaji ambao Mwekezaji Aliyeidhinishwa ametimiza vigezo vilivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii;

"Mtanzania" maana yake ni:

(a) mtu yeyote ambae ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria inayohusiana na uraia; au

(b) kampuni iliyosajiliwa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura ya 212;

"Utalii na burudani" maana yake ni eneo maalum la uchumi lililotangazwa chini ya kifungu cha 35(3) cha Sheria hii, ili kurahisisha utalii na vituo vya burudani, huduma zake na shughuli zinazohusiana nazo;

"Uendeshaji wa majaribio" maana yake ikiwa inahusiana na mradi wa uzalishaji, ni kipindi ambacho Mwekezaji Aliyeidhinishwa anakitumia kufanya uzalishaji wa majaribio na ikiwa ni mradi usio wa uzalishaji ni kipindi cha awali cha kuanza kazi kama inavyothibitishwa na Mamlaka;

"Mzanzibari" maana yake ni:

(a) Mzanzibari kama alivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Mzanzibari; au

(b) Kampuni ambayo imesajiliwa Zanzibar kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ambayo Mamlaka imeridhia kwamba sehemu kubwa ya hisa zake zinamilikiwa na Wazanzibari.

## SEHEMU YA PILI
## MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR

Uanzishwaji wa Mamlaka.

**3.**-(1) Inaanzishwa Mamlaka inayojulikana kama Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar ambayo kwa ufupi itajulikana kama "ZIPA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo chenye kujitegemea, chenye kurithiwa, chenye muhuri wake na kitakuwa na uwezo kwa kupitia jina lake wa:

(a) kuingia mikataba;

(b) kushitaki na kushitakiwa;

(c) kukopa na kupokea mali, pesa ikijumuisha kuwa na fedha zake zenyewe;

(d) kuchukua, kununua au kumiliki kwa njia yoyote au kuhaulisha mali inayohamishika na isiyohamishika; na

(e) kufanyika au kusababisha kufanyika au kutekeleza mambo au vitendo vyote kwa utekelezaji mzuri wa kazi chini ya Sheria hii, kama itavyotekelezwa na Mamlaka.

Madhumuni na malengo ya Mamlaka.

**4.** Madhumuni na malengo ya Mamlaka yatakuwa ni:

(a) kusimamia na kuendesha shughuli za Uwekezaji Zanzibar ikiwemo Maeneo Huru ya Uchumi kwa kuzingatia misingi ya uwazi na ushindani;

(b) kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu inayovutia kwa uwekezaji, kituo cha biashara na eneo la usafirishaji;

(c) kituo kikuu cha ushajiishaji na uwezeshaji uwekezaji na biashara;

(d) kutoa msaada wa kitaasisi kwa maendeleo ya kiuchumi na kuhakikisha uwekaji wa sera za kiuchumi na kibiashara;

(e) kukuza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa ndani au wa nje na kuhakikisha mazingira rafiki ya biashara;

(f) kuwa ni taasisi kuu yenye kuhusika na kuitambulisha Zanzibar kiupekee katika kushajiisha uwekezaji;

(g) kuwezesha uwekezaji wa ndani na wa nje na kuhakikisha mazingira rafiki ya biashara; na

(h) kutoa msaada wa kitaasisi katika kuendeleza na kusimamia Maeneo Huru ya Uchumi.

Kazi za Mamlaka.

**5.** (1) Kazi za Mamlaka zitakuwa ni:

(a) kuishauri Serikali juu ya sera na mikakati sahihi ya kujenga taswira nzuri ya nchi itakayowezesha kuendeleza biashara, kukuza usafirishaji na kutoa huduma kwa wawekezaji;

(b) kuibua na kufanya tafiti na kutumia matokeo ya tafiti hizo na kutayarisha mipango na mikakati ya kuendeleza uwekezaji na biashara;

(c) kwa kushirikiana na wizara husika na mamlaka nyengine, kutayarisha fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini na namna ya kuzifikia;

(d) kuimarisha mazingira ya kibiashara kwa kufanya shughuli nyengine ambazo ni muhimu katika kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu inayovutia kwa uwekezaji na biashara;

(e) kuishauri Serikali juu ya namna na utekelezaji wa vivutio katika uwekezaji na kusimamia matokeo yake;

(f) kuweka, kuendeleza, kujenga, kubadilisha, kuingiza, kudhibiti na kusimamia sehemu za uwekezaji, majengo au ardhi pamoja na vitu vilivyomo katika ardhi hiyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(g) kushauri na kuwezesha maendeleo ya uwekezaji ambayo yana umuhimu mkubwa kwa uchumi wa nchi na kushirikiana na washirika wa maendeleo wa ndani na wa kimataifa ili kuweka uwiano wa aina ya uwekezaji unaofaa;

(h) kusimamia na kusaidia makubaliano ya ubia na ushirikiano juu ya uwekezaji wa wenyeji nje ya nchi;

(i) kusimamia Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji ambacho Mwekezaji Aliyeidhinishwa atapitisha maombi yake yote kwa ajili ya kibali, ruhusa, leseni na huduma nyengine ambazo hazipo chini ya Mamlaka, kufanya uratibu katika taasisi za Serikali au za binafsi ambazo zitakuwa ni muhimu kupitia makubaliano na taasisi au taratibu zilizotajwa katika kutekeleza kanuni au taratibu nyengine zilizowekwa;

(j) kuanzisha na kukuza mashirikiano miongoni mwa taasisi husika za Serikali kuhakikisha utekelezaji wa sheria, taratibu zote zinazotumika pamoja na vigezo vyengine;

(k) kumshauri Waziri juu ya orodha ya shughuli ambazo haziruhusiwi kufanywa na mwekezaji wa ndani ya Zanzibar ikijumuisha shughuli zilizokatazwa na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii; na

(l) kuwa na jukumu la utawala, udhibiti na uwendeshaji wa Maeneo Huru ya Uchumi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kazi za Mamlaka yalioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka katika kutekeleza kazi mahsusi za:

(a) kutekeleza sera na mipango ya Serikali kuhusiana na Maeneo Huru ya Uchumi;

(b) kushajihisha na kuyatangaza Maeneo Huru ya Uchumi kwa waendelezaji wenye muelekeo wa kuwekeza na kwa waendeshaji au wawekezaji wengine;

(c) kufanya kazi za kipekee chini ya masharti yaliyokubaliwa kama yalivyoelekezwa na kanuni zote za uendeshaji wa biashara na huduma zinazotumika katika maeneo yaliyochaguliwa kuwa Maeneo Huru ya Uchumi;

(d) kutunza takwimu zilizopo juu ya utekelezaji na mipango kwa kila Mwekezaji Aliyeidhinishwa;

(e) kuwadhibiti watoa huduma wasiokuwa na leseni kutoka Mipaka ya Forodha kama itakavyohitajika kwa lengo la kutoa huduma kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa;

(f) kuweka miongozo, kutekeleza, kuangalia na kusimamia nyanja zote za utawala wa Maeneo Huru ya Uchumi kama ilivyowekwa katika Sheria hii;

(g) kutunza kumbukumbu za miradi na wakaazi wazawa katika Maeneo Huru ya Uchumi; na

(h) kutoa mapendekezo kwa Waziri katika nyanja zote za kuchagua, kuthibitisha, kuanzisha, kutekeleza na usimamizi wa Maeneo Huru ya Uchumi

(3) Mamlaka itafanya kazi nyengine zozote kwa kadri zitakavyotokezea ambazo zitarahisisha kufikiwa kwa malengo ya Mamlaka au katika kutekeleza uwezo wake.

(4) Kwa kuzingatia Kanuni itakayotungwa chini ya Sheria hii, Mamlaka itaiarifu au itaomba ridhaa kwa Serikali juu ya miradi ya uwekezaji Zanzibar kama itakavyojitokeza.

Uwezo wa Mamlaka.

**6.** Kwa kuzingatia idhini ya Waziri, Mamlaka itakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuweka vigezo na taratibu za maombi ya Cheti cha Uwekezaji kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa pamoja na Uwekezaji Mkakati kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii;

(b) kuweka utaratibu wa utoaji vivutio kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa ikijumuisha Uwekezaji Mkakati kama ilivyoanishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii;

(c) kuweka utaratibu na vigezo vya maombi kwa Uwekezaji Mkakati kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii;

(d) kuweka aina ya cheti, kibali au leseni itakayotolewa kwa mujibu wa Sheria hii;

(e) kuweka muda ambao Mamlaka itatoa uamuzi wa kukubali au kukataa kutoa au kufuta cheti, kibali au leseni na utaratibu wa ubadilishaji wake;

(f) kuainisha kodi, tozo na ada kwa huduma yoyote itakayotolewa na Mamlaka au kwa utoaji wa cheti, kibali au leseni kwa mtu yeyote;

(g) kuainisha taasisi za Serikali ambazo zitaunda Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji;

(h) kushauri juu ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(i) kuainisha, kuliwekea ramani na itakapolazimu kutafuta waendelezaji na waendeshaji wa maeneo ya ardhi itakayotumika au iliyotengwa kwa ajili ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(j) kuainisha utaratibu wa ukodishaji wa ardhi na kutoa hati ya umiliki kwa ardhi au mali yoyote kwa mwendelezaji, mwendeshaji au mtoa huduma au Mwekezaji Aliyeidhinishwa yeyote anaewekeza katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(k) kuainisha utaratibu wa kutekeleza au kuidhinisha uendelezaji, uendeshaji au usimamizi au ufadhili kwa miundombinu inayofaa kutoka katika mipaka au ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi yaliyochaguliwa wakati itakapohitajika kufanya hivyo;

(l) kuhakikisha Maeneo Huru ya Uchumi yanaendelezwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa; na

(m) kuweka utaratibu wa kuainisha ardhi iliyotengwa kwa uwekezaji nje ya Maeneo Huru ya Uchumi.

Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji.

**7.**-(1) Mamlaka itafanyakazi kama ni Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji ambapo kitatoa huduma zinazohitajika kwa Wawekezaji Walioidhinishwa.

(2) Lengo la Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji litakuwa ni kuwezesha upatikanaji wa huduma zinazohitajika kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza biashara yake kwa haraka zaidi.

(3) Katika kutekeleza majukumu yake kama Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji, Mamlaka itakuwa na maofisa waandamizi kutoka Kamisheni ya Ardhi, Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi, Wakala wa Majengo Zanzibar, Mamlaka ya Mazingira Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Idara ya Udhibiti Ujenzi na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar.

(4) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi, kuongeza au kupunguza taasisi yoyote iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki.

(5) Bila kujali sheria nyengine yoyote, Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji kwa ajili ya kuwezesha utaratibu wa maombi kwa usajili, kibali, leseni, ruhusa inayohitaji kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki:

(a) kitapokea maombi yote kutoka kwa Wawekezaji kwa uandikishaji au kibali chochote, leseni, ruhusa chini ya sheria yoyote na kuwasilisha maombi katika taasisi ya umma inayohusika; na

(b) kitahakikisha kwamba maombi yoyote yanafanyiwa kazi kwa haraka na taasisi ya umma inayohusika.

(6) Endapo maombi yatakuwa hayajashughulikiwa ndani ya kipindi kilichoainishwa katika Jadweli lililoundwa chini ya Sheria hii, taasisi ya umma, haraka iwezekanavyo na si zaidi ya siku tatu za kazi tokea kipindi hicho kilichoanishwa, itamjuulisha Mkurugenzi Mtendaji sababu ambazo maombi hayo kutokushughulikiwa;

(7) Baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mtendaji atamjuulisha Mwekezaji na ataainisha sababu na anaweza kupendekeza kwa taasisi ya umma husika kama atavyoona inafaa na taasisi hizo za umma zitapaswa kuyatekeleza mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA MAMLAKA

Uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi.

**8.** (1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambae atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji;

(c) Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango;

(d) Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Zanzibar.

(e) Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi; na

(f) Wajumbe wengine wawili watakaoteuliwa na Waziri mmoja kati yao atakuwa mwakilishi wa sekta binafsi na kwa kuzingatia jinsia.

(2) Mtu yeyote atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe aliyeteuliwa chini ya aya (f) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu ya angalau shahada ya kwanza katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, fedha, ujasiriamali wa kiviwanda, sheria au fani nyengine zinazolingana na hizo;

(c) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano kwa Mjumbe na miaka kumi kwa Mwenyekiti katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, fedha, ujasiriamali wa kiviwanda, sheria au fani nyengine zinazolingana na hizo; na

(d) hajihusishi moja kwa moja na shughuli zozote za kisiasa.

(3) Bodi itateua ofisa wa umma ambae atakuwa muajiriwa wa Mamlaka mwenye sifa na anayefaa kuwa Katibu wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

**9.** Isipokuwa kwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti wa Bodi atatumikia kwa kipindi cha miaka minne na wajumbe wengine wa Bodi watatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu lakini wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Akidi

**10.** Akidi ya kikao chochote cha Bodi itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe.

Utaratibu wa vikao.

**11.** Bodi itaandaa utaratibu wa uendeshaji wa vikao vyake.

Vikao vya Bodi.

**12.**-(1) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Bodi na ikiwa hayupo, wajumbe waliohudhuria katika kikao watachagua mjumbe miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

(2) Bodi itakutana kwa vikao vya kawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kuitisha kikao cha dharura endapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Maamuzi.

**13.**-(1) Maamuzi ya Bodi yatafikiwa kwa njia ya makubaliano.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, endapo Bodi itashindwa kufikia makubaliano, maamuzi yatafanywa kwa wingi wa kura za Wajumbe.

(3) Endapo kutakuwa na uwiano wa kura, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Posho la wajumbe.

**14.** Wajumbe wa Bodi watastahili kulipwa posho kama Waziri atakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mjumbe mualikwa.

**15.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika vikao vyake lakini mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Ukomo wa wajumbe.

**16.**-(1) Mjumbe wa Bodi atasita kutumikia nafasi yake ikiwa:

(a) hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kumjulisha Mwenyekiti;

(b) atathibitishwa na mamlaka inayohusika kuwa mgonjwa wa akili au ana ugonjwa mwengine utakaomfanya ashindwe kutekeleza majukumu yake;

(c) atajiuzulu na kutoa taarifa katika mamlaka ya uteuzi na akaijuilisha sababu za kujiuzulu kwake;

(d) atatangazwa kuwa amefilisika;

(e) atahukumiwa kifungo kwa kipindi cha miezi sita au zaidi;

(f) atashindwa kuweka wazi maslahi yake juu ya jambo linalojadiliwa katika kikao;

(g) uteuzi wake utasitishwa na mamlaka iliyomteua; au

(h) atafariki.

(2) Waziri anaweza, kwa kuzingatia sababu zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kutengua uteuzi wa mjumbe aliyemteua.

Uwezo na kazi za Bodi.

**17.** Bodi itakuwa na kazi na uwezo wa:

(a) kutoa maelekezo halali kwa Mkurugenzi Mtendaji katika utendaji, sera za utendaji na utekelezaji wa Mamlaka;

(b) kuanzisha muundo wa taasisi na utaratibu wa kazi kama itakavyoona inafaa kwa utekelezaji wa kazi na majukumu ya Mamlaka;

(c) kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, kuainisha vigezo na masharti ya utumishi, mishahara, mafao kwa wafanyakazi wa Mamlaka;

(d) kuweka mpango kazi, malengo na dhamira sahihi ya kazi kwa kila idara ya Mamlaka na kusimamia hatua zilizofikiwa;

(e) kuainisha mikakati au sera zinazoongoza utekelezaji wa Mamlaka;

(f) kuteua kamati ambayo wajumbe wake watakuwa ni wale wale wajumbe wa Bodi au wajumbe wengine ambao imekasimu uwezo wake kadri itakavyoonekana inafaa;

(g) kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, kuanzisha kanuni za watumishi na fedha;

(h) kutoa miongozo ya jumla katika sekta za kipaumbele za uwekezaji kwa kuzingatia maeneo yenye manufaa zaidi kwa Zanzibar;

(i) kwa kuzingatia Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii, kuidhinisha vigezo na viwango vya mtaji wa uwekezaji;

(j) kufuatilia ipasavyo maendeleo ya Miradi iliyoidhinishwa;

(k) kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 25(5) cha Sheria hii, kuthibitisha ufutwaji wa Cheti cha Uwekezaji; na

(l) kuwa ni chombo cha mwanzo cha rufaa kwa Mwekezaji yeyote Aliyeidhinishwa ambae hakuridhika na maamuzi.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**18.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambae atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ndie mtendaji mkuu wa Mamlaka na atasimamia utekelezaji wa kazi za kila siku za Mamlaka.

(3) Mtu atateuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji, iwapo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) anayo elimu ya angalau shahada ya kwanza katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, uongozi, uhusiano wa kimataifa, ujasiriamali wa kiviwanda, sheria au fani nyengine zinazolingana na hizo; na

(c) anao uzoefu wa kazi usiopungua miaka kumi katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, uongozi, uhusiano wa kimataifa, ujasiriamali wa kiviwanda, sheria au fani nyengine zinazolingana na hizo;

(4) Bila ya kuathiri uwezo wa Waziri au Bodi waliopewa kwa mujibu wa Sheria hii, uwezo na kazi za Mamlaka zilizowekwa chini ya Sheria hii zitatekelezwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa niaba ya Mamlaka.

Watendaji wa Mamlaka.

**19.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma katika kupitisha muundo wa utumishi wa Mamlaka na ngazi za watendaji:

(a) Bodi itateua Wakurugenzi wa Idara na Maofisa Wakuu wa Mamlaka; na

(b) Mkurugenzi Mtendaji kwa kushauriana na Bodi, anaweza kuajiri maofisa wengine na wafanyakazi kwa kadri itakavyolazimu ili kurahisisha ufanikishaji wa majukumu na kazi za Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## HAKI, WAJIBU NA MAKATAZO KWA WAWEKEZAJI

Haki ya mwekezaji.

**20.**-(1) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya sheria yoyote, shughuli zote za biashara zitakuwa wazi kwa mwekezaji yeyote isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mwekezaji anaweza kushawishiwa kuwekeza katika sekta za kipaumbele kama zitakavyotangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi muda baada ya muda.

(3) Waziri anaweza, chini ya Jadweli la Nne la Sheria hii, kuainisha baadhi ya shughuli za kibiashara kuwa zimewekwa maalum kwa wazanzibari.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, katazo hilo halitohusisha uwekezaji ambazo tayari umeidhinishwa na kuruhusiwa awali.

(5) Kasino, kamari au biashara yoyote ya bahati nasibu hairuhusiwi Zanzibar.

Wajibu wa Mwekezaji Aliyei-dhinishwa.

**21.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa atalazimika:

(a) kuwekeza si chini ya kiwango cha mtaji kilichothibitishwa na Mamlaka na kufafanuliwa katika cheti cha uwekezaji kilichotolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii;

(b) kutekeleza mradi ulioidhinishwa kwa mujibu wa mpango kazi, upembuzi yakinifu au mpango wa utekelezaji ulioidhinishwa na Mamlaka;

(c) kufungua hesabu ya fedha za kitanzania au fedha za kigeni kwa kadri atakavyoona inafaa katika benki yoyote ndani ya Zanzibar na atafanya miamala yake ya kibiashara kupitia hesabu hiyo;

(d) Mwekezaji Aliyeidhinishwa atakayehitaji kufungua hesabu nje ya Zanzibar inayohusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa, atalazimika kupata ruhusa ya maandishi kutoka Mamlaka kabla ya kufungua hesabu hiyo;

(e) kujisajili kwenye taasisi za kodi, kuwasilisha marejesho ya kodi kwa wakati, kulipa kodi zote anazostahiki na kuomba vivutio vya kodi;

(f) kuweka vizuri taarifa za fedha na za hesabu za uwekezaji ulioidhinishwa na kuwasilisha kivuli cha hesabu iliyokaguliwa kwa Mamlaka, ndani ya miezi sita ya mwaka wa fedha unaofuata;

(g) kuomba mwanzo idhini kutoka Mamlaka juu ya mabadiliko yoyote ya jina, uongozi, umiliki, uhaulishaji wa hisa na pale mabadiliko mengine yoyote au uhaulishaji umefanywa bila ya kupatikana kwanza idhini ya Mamlaka, mmiliki mpya, uongozi au muhaulishwaji atachukuliwa kwamba amekubali na ameridhia majukumu yote;

(h) kutunza kumbukumbu zote zinazohusiana na uendeshaji wake kwa muda wa miaka mitano;

(i) kuwaruhusu maofisa wa Mamlaka wakati wa kutekeleza majukumu yao ya ufuatiliaji;

(j) kutoa taarifa kwa wakati anapotakiwa na mamlaka za Serikali;

(k) kuwasilisha kwa wakati ripoti za utekelezaji kazi za robo mwaka wakati wa uendelezwaji na uendeshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa;

(l) kukata upya leseni, cheti au kibali kinachohitajika katika utekelezaji au uendeshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa kwa wakati;

(m) kuruhusu ofisa wa Serikali au wakala wake aliyeruhusiwa kuingia katika eneo na kufanya ukaguzi wa maeneo, mabuku, kumbukumbu au nyaraka nyengine zozote;

(n) kuijuilisha Mamlaka, mabadiliko yoyote yanayohusiana na maelezo ya cheti, ukomo wa utekelezaji, mabadiliko ya umiliki wa hisa au jambo jengine lolote linalohusiana na mabadiliko ya utekelezaji; na

(o) kufuata masharti ya Sheria hii, sheria za mazingira na sheria nyengine zozote zinazotumika Zanzibar.

Katazo.

**22.** Mwekezaji anakatazwa:

(a) kuahidi, kushawishi au kutoa rushwa kwa mtumishi yeyote wa umma;

(b) kutafuta na kupata ardhi ya uwekezaji kutoka kwa jamii isipokuwa kwanza apate idhini kutoka mamlaka inayohusika;

(c) kukwepa kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria hii;

(d) kutoa maelezo ya uongo, kutoa makisio yaliyo chini ya kiwango sahihi au kuficha mapato, thamani au faida au kutoa makisio ya juu kudai vivutio asivyostahiki;

(e) kutoa tuhuma za uongo au kusambaza propaganda dhidi ya taasisi za Serikali au maafisa wake;

(f) kufungua hesabu ya fedha za kigeni nje ya Tanzania bila kupata ridhaa ya kimaandishi ya Mamlaka; au

(g) kuvunja au kutotii sheria au kanuni zozote zinazotumika Zanzibar.

## SEHEMU YA TANO
## UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA

Maombi ya Cheti cha Uwekezaji.

**23.**-(1) Raia wa kigeni ambae amewekeza au anatarajia kuwekeza, atalazimika kuomba kwa Mamlaka Cheti cha Uwekezaji na mradi huo utatambulika kuwa ni Mradi wa Mgeni Ulioidhinishwa kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Mzanzibari au Mtanzania ambaye amewekeza au anatarajia kuwekeza Zanzibar, atalazimika kuomba kwa Mamlaka Cheti cha Uwekezaji kwa mradi kuwa Kampuni iliyowekeza au inayotarajiwa kuwekeza, itatambulika kuwa ni Mradi ulioidhinishwa wa Mwenyeji kwa madhumuni ya Sheria hii.

(3) Mamlaka itazingatia kila ombi lililowasilishwa kwa mujibu wa kifungu hiki na ikiwa itaridhika kwa hali yoyote kuwa:

(a) ni uwekezaji au uwekezaji unaotarajiwa kuwekezwa ambao mali au thamani isiyopungua kiwango ambacho kimepangwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) uwekezaji au uwekezaji unaotarajiwa kuwekezwa umekamilisha vigezo vya ziada vilivyoainishwa kwa mujibu wa Sheria hii;

inaweza kutoa Cheti cha Uwekezaji kwa muombaji.

(4) Mamlaka itachukua uamuzi wa kutoa au kutokutoa Cheti cha Uwekezaji, na kumjulisha muombaji juu ya uamuzi huo katika muda uliopangwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Yanayotakiwa kuwemo katika Cheti cha Uwekezaji.

**24.** Cheti cha Uwekezaji kinajumuisha mambo yaliyoelezwa katika Jadweli la Tano la Sheria hii.

Kusitisha na kufuta Cheti cha Uwekezaji.

**25.**-(1) Mamlaka inaweza kusitisha Cheti cha Uwekezaji kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 23(3) cha Sheria hii, ikiona kwamba:

(a) Cheti cha Uwekezaji kimepatikana kwa njia ya udanganyifu;

(b) Cheti cha Uwekezaji kimepatikana kutokana na taarifa za kupotosha;

(c) Mwekezaji Aliyeidhinishwa yupo katika hatua za kufunga biashara;

(d) Mwekezaji Aliyeidhinishwa ameshindwa kuanza utekelezaji ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kupata nyaraka zote za kisheria;

(e) mradi umetelekezwa;

(f) Mwekezaji Aliyeidhinishwa ameomba vivutio ambavyo vimetolewa chini ya Sheria hii, na kuvitumia kinyume na matakwa ya Sheria;

(g) Mwekezaji Aliyeidhinishwa ameshindwa bila ya sababu za msingi kuanza shughuli ndani ya muda uliowekwa kwenye Cheti cha Uwekezaji;

(h) Mwekezaji Aliyeidhinishwa ameshindwa kutekeleza wajibu wowote uliowekwa kwa mujibu wa Sheria hii; au

(i) Mwekezaji Aliyeidhinishwa amefanya shughuli yoyote ambayo imekatazwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(e) cha kifungu hiki, mradi utahesabiwa kuwa umetelekwezwa ikiwa:

(a) mwekezaji ameondoka nchini na ameuacha mradi bila ya taarifa kwa watu wake wa karibu; na

(b) baada ya Mamlaka kufanya jitihada ya kumtafuta mwekezaji ndani ya kipindi cha miezi sita na jitihada hizo kushindikana.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka itatoa indhari ya angalau siku thelathini kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa kutoa sababu kwanini Cheti cha Uwekezaji alichopewa kisifutwe.

(4) Pale ambapo Mwekezaji Aliyeidhinishwa ametoa maelezo ya kuiridhisha Mamlaka, Mamlaka itaondosha sitisho na kumuongoza mwekezaji namna itakavyoona inafaa.

(5) Endapo Mwekezaji Aliyeidhinishwa:

(a) atashindwa kutimiza masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki;

(b) ametoa maelezo yasiyoridhisha kwa Mamlaka; au

(c) atauondoa Uwekezaji Ulioidhinishwa;

Mamlaka itafuta Cheti cha Uwekezaji.

Athari za kufutwa kwa Cheti.

**26.** Pale endapo Mamlaka imefuta Cheti cha Uwekezaji, kilichotolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii:

(a) uwekezaji huo utasita kutambulika kuwa ni Uwekezaji Ulioidhinishwa;

(b) mkataba wa ukodishaji wa ardhi unaohusiana na Cheti cha Uwekezaji utafutika papo hapo; na

(c) vivutio vya kodi vinavyotolewa chini ya Sehemu ya Sita ya Sheria hii, vitasita na kodi zote zilizokuwa zimesamehewa zitalazimika kulipwa ipasavyo.

Marekebisho ya Cheti.

**27.**-(1) Mamlaka inaweza, kwa maombi ya Mwekezaji Aliyeidhinishwa, kurekebisha Cheti cha Uwekezaji endapo:

(a) kumekuwa na haja ya kuongeza muda wa ziada katika utekelezaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa;

(b) jina la mradi litabadilishwa na kuwa jina jengine;

(c) mwekezaji mwengine amefanikiwa kujiunga katika mradi wa Mwekezaji Aliyeidhinishwa;

(d) mtaji zaidi unawekezwa na Mwekezaji Aliyeidhinishwa au Mwekezaji Mwengine; au

(e) haki katika mradi zimekwenda kwa mwekezaji mwengine kutokana na kifo cha Mwekezaji Aliyeidhinishwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mwekezaji Aliyeidhinishwa atalazimika, ndani ya kipindi kisichozidi siku thelathini, kuijulisha Mamlaka kwa maandishi juu ya mabadiliko na atawasilisha nyaraka zilizotajwa ndani ya Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

(3) Mmiliki wa Cheti cha Uwekezaji atalazimika kulipa ada zilizoainishwa na Mamlaka kama **zitakavyoelezwa** ndani ya Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA SITA
## FURSA NA VIVUTIO VYA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA

Upatikanaji wa leseni, vibali na huduma nyengine.

**28.** Iwapo Mwekezaji Aliyeidhinishwa amepewa Cheti cha Uwekezaji, Mamlaka itasimamia, kwa maombi ya mwekezaji, upatikanaji wa leseni, vibali na huduma nyengine muhimu zitakazohitajika.

Ajira kwa wataalamu wageni.

**29.**-(1) Katika Mradi wowote Ulioidhinishwa, ajira zitatolewa kwa Watanzania lakini kipaumbele kitakuwa kwa Wazanzibari.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaweza kuajiri mtaalamu wa kigeni katika nafasi muhimu pale ambapo hakupatikana Mtanzania mwenye sifa hiyo baada ya kutangazwa kwa nafasi hiyo.

(3) Idadi ya wataalamu wa kigeni chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itaamuliwa na Mamlaka baada ya kushauriana na Kamisheni ya Kazi.

Upatikanaji wa ardhi.

**30.**-(1) Pale ambapo Mwekezaji Aliyeidhinishwa atahitaji ardhi iliyo nje ya Maeneo Huru ya Uchumi, Mamlaka itapeleka maombi kwa waziri anaehusika na ardhi na kupendekeza masharti ya ziada yatakayowiana na aina ya uwekezaji.

(2) Iwapo ardhi iliyopatikana chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki imehodhiwa na mtu mwengine, Mwekezaji Aliyeidhinishwa atalazimika kumfidia kwa haraka na kwa usahihi kwa njia ya fedha au kiwango sahihi cha Hisa za Upendeleo katika mradi huo kwa uendelezaji utaofanywa au faida zitakazotokana na ardhi hiyo.

Vivutio na ruhusa.

**31.**-(1) Mwekezaji Aliyeidhinishwa atastahiki kupatiwa vivutio na misamaha kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kodi au sheria nyengine yoyote inayotumika Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mwekezaji Mkakati anaweza pia kupatiwa fursa, vivutio na ruhusa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Sita la Sheria hii.

(3) Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaweza pia kupatiwa vivutio na ruhusa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Saba la Sheria hii.

(4) Mamlaka, baada ya kushauriana na taasisi husika, inaweza kupendekeza kwa Waziri fursa na vivutio kwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae amewekeza au anataka kuwekeza katika uwekezaji uliovumbuliwa au uwekezaji katika maeneo ambayo kijografia sio mazuri kwa uwekezaji.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Mamlaka inaweza kukataa kumpatia baadhi ya fursa, ruhusa au vivutio Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae ameshindwa kufuata sharti lolote lililotolewa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA SABA
## DHAMANA KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA

Haki ya kuhaulisha fedha.

**32.** Bila kujali masharti ya Sheria nyengine yoyote, mgeni aliyewekeza Zanzibar anaweza baada ya kulipa kodi, kuhaulisha fedha nje ya Zanzibar kwa kutumia fedha za kigeni zinazobadilishika kwa viwango vya ubadilishaji fedha vilivyokuwepo:

(a) gawio linalotokana na uwekezaji au nje ya uwekezaji wake kwa mali za kigeni;

(b) mtaji na riba zitakazotokana na mkopo wowote wa nje unaohusiana na uwekezaji uliosajiliwa Zanzibar;

(c) mapato yanayotokana na ufilisi au mauzo ya uwekezaji au sehemu ya hizo; na

(d) bidhaa nyengine yoyote ya matumizi mengine yoyote ya kigeni inayohusiana na uwekezaji.

Kinga dhidi ya kuchukuliwa mali kwa lazima.

**33.**-(1) Hakuna Mradi Ulioidhinishwa au Mradi wa Mwenyeji Ulioidhinishwa au mali ya Mwekezaji yeyote ambayo itachukuliwa kwa lazima, na hakuna hisa au haki juu ya Mradi kama huo au mali zake ambazo zitachukuliwa kwa lazima isipokuwa kwa kufuata masharti ya kulipwa fidia inayofaa na ya kutosha kama ilivyoelezwa na kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

(2) Iwapo uchukuwaji wa lazima utafanywa kwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) amri iliyotolewa na kutiwa saini na Waziri itachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali; na

(b) kabla ya uchukuaji kufanywa utaratibu wa haraka utafanywa wa kutathmini na kulipa fidia ya kutosha na ya haki.

Utatuzi wa migogoro.

**34.**-(1) Endapo Mwekezaji hajaridhika na fidia iliyotolewa chini ya kifungu 33(1) cha Sheria hii, au ikiwa migogoro imetokezea baina ya Mwekezaji huyo na Mamlaka kuhusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa, jitihada zitafanywa ili kusuluhisha migogoro hiyo kwa njia ya amani.

(2) Mgogoro wowote baina ya Mwekezaji na Mamlaka unaohusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa ambao haujatatuka katika njia ya majadiliano, unaweza kuwasilishwa kwa usuluhishi kwa mujibu wa:

(a) kanuni na taratibu zilizowekwa chini Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25 ya Sheria za Zanzibar;

(b) mfumo wa makubaliano ya pande mbili au zaidi juu ya ulinzi wa uwekezaji uliokubalika baina ya Serikali na Serikali ambayo Mwekezaji anatoka; au

(c) kanuni na taratibu za usuluhishi chini ya Tume ya Usuluhishi ya Kimataifa za Sheria ya Biashara ya Kimataifa zinazotumika wakati cheti kilipotolewa au Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji.

(3) Hakuna jambo katika kifungu hiki litakalomzuia Mwekezaji Aliyeidhinishwa na Mamlaka kukubaliana kwamba mgogoro wowote utakaotokezea, hautopelekwa katika Mahakama za Ushuluhishi za Kimataifa lakini ni vyema kusikizwa na kumalizwa kwanza na Mahakama zenye mamlaka hapa Zanzibar.

## SEHEMU YA NANE
## MAENEO HURU YA UCHUMI

Utambuzi na utangazaji wa Maeneo Huru ya Uchumi.

**35.**-(1) Maeneo Huru ya Uchumi yatajumuisha Eneo la Fumba, Eneo la Viwanda Amani, Eneo la Maruhubi na Eneo la Uwanja wa Ndege kwa Unguja na Eneo la Micheweni kwa Pemba kama yalivyotangazwa kwa Amri ya Rais Namba 5 na Namba 29 za 1993, Namba 61 ya 2000 na Namba 14 ya 2004.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Rais anaweza kutangaza kupitia Amri katika Gazeti Rasmi, eneo jengine lolote Unguja au Pemba kuwa ni Eneo Huru la Uchumi kwa madhumuni ya Sheria hii na anaweza kuainisha mipaka na kuyapa majina maeneo hayo.

(3) Eneo lililotangazwa kuwa Eneo Huru la Uchumi linaweza kuwa:

(a) limetengwa kwa matumizi ya sekta maalum au sekta mchanganyiko za Maeneo Huru ya Uchumi na yanaweza kujumuisha, lakini hayaishii kwa:

(i) Eneo Huru la Biashara;

(ii) Eneo la Viwanda;

(iii) Bandari Huru;

(iv) Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

(v) Eneo la Sayansi na Teknolojia;

(vi) Eneo la Kilimo;

(vii) Eneo la Mifugo;

(viii) Eneo la Uvuvi;

(ix) Eneo la Utalii na Burudani;

(x) Eneo la Huduma za Biashara; au

(xi) Eneo la Kumbi za Mikutano.

(b) limeendelezwa ikiwa na sekta ya umma, sekta binafsi au kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi au kwa njia nyengine yoyote ya ubia, endapo bidhaa zozote zimeingizwa na huduma zake zimeainishwa zitatozwa ushuru na kodi ya uingizaji kama zipo nje ya Mipaka ya Forodha na endapo kuna faida inatolewa, itatolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

(4) Ardhi yoyote iliyotangazwa kuwa ni Eneo Huru la Uchumi haitotumika kwa matumizi binafsi.

(5) Taratibu na usimamizi wa shughuli ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi yatafanywa kwa kuzingatia misingi ya uwazi na ushindani.

(6) Waziri anaweza kutunga Kanuni juu ya jambo lolote linalohusiana na Maeneo Huru ya Uchumi ambayo usimamizi wake unahitaji kuwekewa Kanuni.

Malengo na madhumuni.

**36.** Malengo na madhumuni ya Maeneo Huru ya Uchumi ni:

(a) kuwawekea wawekezaji upeo mpana wa utekelezaji, kuwawekea masharti bora ya utekelezaji na kuwahakikishia maeneo thabiti ya biashara ikijumuisha:

(i) kuendelea kuweka miundombinu inayohitajika;

(ii) kuanzisha vivutio kwa ajili ya shughuli za biashara na uchumi katika maeneo yaliyotengwa kuwa Maeneo Huru ya Uchumi; na

(iii) kuondosha vikwazo vyote kwenye shughuli za kiuchumi na biashara zenye tija zinazofanyika katika maeneo hayo.

(b) kurahishisha maendeleo ya teknolojia katika fani maalum na kukuza uzalishaji kwa ajili ya usafirishaji wa nje;

(c) kuvutia huduma za kimataifa; na

(d) kuzalisha ajira kwa wenyeji.

Kutambuliwa bidhaa kuwa imeingizwa au imesafirishwa nje ya nchi.

**37.** Isipokuwa imeelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au sheria nyengine yoyote:

(a) bidhaa itakayotoka ndani ya eneo lolote la udhibiti wa forodha na kuingizwa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi au huduma iliyotolewa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi kutoka eneo jengine la udhibiti

wa forodha, bidhaa na huduma hizo zitahesabiwa zimetoka nje ya nchi; na

(b) Bidhaa zitakazotoka ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi na kupelekwa katika eneo jengine la udhibiti wa forodha au huduma itakayotolewa kutoka Maeneo Huru ya Uchumi kwenda eneo jengine la udhibiti wa forodha, zitahisabiwa kuwa zimeingizwa nchini kutoka nchi nyengine.

Bidhaa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi.

**38.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii pamoja na Sheria za Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki, bidhaa na huduma ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi zinaweza:

(a) kuhifadhiwa, kuuzwa, kuoneshwa, kupanguliwa, kufungashwa upya, kuunganishwa, kusambazwa, kupembuliwa, kuwekwa viwango, kusafishwa, kuchanganywa au kuzalishwa au kutengenezwa vyenginevyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(b) kuharibiwa chini ya usimamizi wa ofisa stahiki; au

(c) kuondoshwa chini ya usimamizi wa ofisa stahiki kutoka Maeneo Huru ya Uchumi kwa ajili ya usafirishaji nje au kupelekwa sehemu nyengine ya Maeneo Huru au kwenye ghala la bidhaa, ambazo hazijalipiwa ushuru aidha zikiwa katika vifungashio vyake vya asili au vyenginevyo.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii pamoja na Sheria za Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki, bidhaa yenye maelezo yoyote ambayo yanaweza kutumika katika shughuli za biashara zilizopata leseni katika maeneo huru zinaweza kuingizwa katika Maeneo Huru ya Uchumi.

(3) Mradi wa Maeneo Huru ya Uchumi utatekelezwa kwa kufuata utaratibu maalum uliotolewa chini ya masharti mahsusi ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki.

Uhamishaji wa bidhaa kutoka Maeneo Huru ya Uchumi.

**39.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 38 cha Sheria hii:

(a) Bidhaa au huduma zilizomo ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi, ambayo yatajumuisha Maeneo ya Usimamizi wa Forodha, hayawezi kuondolewa katika maeneo hayo isipokuwa kwa:

(i) usafirishaji nje;

(ii) kuingia ndani ya mipaka ya forodha kwa masharti ya kanuni, taratibu za forodha;

(iii) kuondoshwa na kupelekwa sehemu yoyote iliyo chini ya usimamizi wa forodha kwa ruhusa ya ofisa maalum wa forodha na kwa kuzingatia masharti yoyote yatakayowekwa; au

(iv) ukarabati, matengenezo au kuchakata au kubadilisha kwa kupata idhini kwanza ya ofisa maalum wa forodha na kwa kufuata masharti yoyote yatakayowekwa.

(b) Iwapo bidhaa zimetengenezwa nje ya Zanzibar, bidhaa hizo zitawekwa alama ya wazi inayoonesha kuwa wapi bidhaa hizo zimetengenezwa;

(c) Huduma zinazotolewa na mradi uliopo katika Maeneo Huru ya Uchumi zinaweza kutolewa kwa:

(i) watu waliopo nje ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania;

(ii) mradi mwengine uliopo katika Maeneo Huru ya Uchumi ikiwa ni mwendelezo wa shughuli za kusafirisha nje ya nchi kwa mradi huo kwa masharti ya kupata ruhusa ya Mamlaka; au

(iii) watu waliopo katika Mipaka ya Forodha kwa masharti ya kupata ruhusa ya Mamlaka.

Eneo la Forodha.

**40.** Maeneo Huru ya Uchumi yaliyotangazwa katika Sheria hii yatazingatiwa kuwa yapo nje ya maeneo ya forodha ambapo Sheria na Kanuni za forodha zinazohusiana na kodi za uingizaji hazitotumika.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Mamlaka.

**41.**-(1) Fedha za Mamlaka zitajumuisha:

(a) ruzuku kutoka Serikalini;

(b) fedha zozote zitakazopatikana kwa malipo ya ukodishwaji kama yalivyoelezwa na Kanuni iliyotungwa chini ya Sheria hii;

(c) fedha zote zitakazopokelewa na Mamlaka kwa utekelezaji wake kutoka vyanzo vyengine vyovyote; na

(d) michango, msaada, zawadi, **wasia** au mikopo inayoweza kupokelewa kihalali kutoka katika taasisi au jumuiya yoyote.

(2) Fedha za Mamlaka zitatumika kulipia gharama na matumizi ya Mamlaka kuhusiana na utekelezaji wa kazi na malengo yake chini ya Sheria hii.

Bajeti ya mwaka.

**42.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mamlaka itaandaa bajeti yake ya mwaka na kuiwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(2) Fedha yoyote ya ziada itakayoidhinishwa na Waziri itarejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Hesabu na ukaguzi.

**43.**-(1) Mamlaka itaweka kumbukumbu ya vitabu vya hesabu vya mapato na matumizi, mali na madeni na shughuli nyengine za Mamlaka na itatayarisha taarifa za hesabu ya mwaka baada ya kukamilika mwaka wa fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha.

(2) Taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI MENGINEYO

Utunzaji siri.

**44.** Bila kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, taarifa zitakazotolewa na mmiliki wa Cheti cha Uwekezaji zitabaki kuwa siri kwa Mamlaka na mtumishi au ofisa wa Mamlaka hawatotoa taarifa hizo kwa mtu yeyote isipokuwa:

(a) kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

(b) akitakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria; au

(c) akitakiwa kufanya hivyo kwa amri ya mahakama au Waziri.

Rufaa.

**45.** Mwekezaji yeyote ambae hakuridhika na uamuzi wowote uliofanywa chini ya Sheria hii, anaweza kukata rufaa kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Mradi uliotelekezwa.

**46.**-(1) Bila kujali masharti ya sheria yoyote, endapo Mamlaka itahisi kuwa mradi umetelekezwa kwa muda wa mwaka mmoja, Mamlaka inaweza:

(a) kutangaza mradi huo kuwa umetelekezwa kupitia katika Gazeti Rasmi;

(b) kusimamia uwekezaji uliotelekezwa au mali;

(c) kusitisha huduma zote za uwekezaji kwa mradi huo; na

(d) kumteua mtu atakaepokea mradi uliotelekezwa.

(2) Mpokeaji aliyeteuliwa chini ya kifungu hiki, atafanya shughuli za kupokea mradi kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Makampuni ya Zanzibar.

Makosa na adhabu.

**47.** Mtu ambae:

(a) atatoa taarifa za uongo au atatoa taarifa za kupotosha kwa Mamlaka;

(b) atakataa au kudharau kutoa taarifa ambazo Mamlaka inazihitaji kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

(c) atakataa kumruhusu ofisa wa Mamlaka kuingia katika eneo la mradi au bishara yake;

(d) atamzuia ofisa yeyote kutekeleza majukumu yake halali aliyopewa chini ya Sheria hii;

(e) atatumia vibaya vivutio au fursa zinazotolewa chini ya Sheria hii;

(f) atafungua hesabu za kigeni nje ya Tanzania zinazohusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa bila ya ruhusa ya maandshi ya Mamlaka;

(g) atashindwa kufuata majukumu kama yalivyotolewa chini ya Sheria hii; au

(h) amefanya jambo lolote ambalo limekatazwa chini ya Sheria hii,

atakuwa amefanya kosa na atakapotiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopungua Dola za Kimarekani Elfu Kumi au sawa na thamani ya Shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

Kanuni.

**48.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa utekelezaji mzuri wa malengo au majukumu ya Sheria hii.

(2) Bila **ya** kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri atatunga Kanuni juu ya:

(a) vigezo na utaratibu wa kuijuilisha au kuiomba idhini Serikali juu ya Mradi wa Uwekezaji;

(b) utoaji wa vivutio maalum kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi ambao watataka kuwekeza Zanzibar; na

(c) utaratibu wa ukataji wa rufaa kwa Mwekezaji yeyote asiyeridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Sheria hii.

(3) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kufuta, kubadilisha au kurekebisha Jadweli lolote chini ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**49.**-(1) Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Namba 11 ya mwaka, 2004 inafutwa.

(2) Jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

---

## VIGEZO NA TARATIBU ZA MAOMBI YA UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA

**[Chini ya kifungu cha 6(a)]**

---

**1.** Mwekezaji Mgeni ataomba Cheti cha Uwekezaji kwa Mamlaka kitakachotolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii baada ya kukamilisha vigezo vifuatavyo:

(a) kuwekeza au anatarajia kuwekeza mtaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni Mbili na Laki Tano kwa miradi ya hoteli na majengo, au zisizopungua Dola za Kimarekani Laki Tatu kwa miradi mengine; na

(b) kufanya biashara za halali kama zilivyowekwa katika Sheria hii.

**2.** Mwekezaji Mzanzibari au Mtanzania ataomba Cheti cha Uwekezaji kwa Mamlaka kitakachotolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii, baada ya kukamilisha vigezo vifuatavyo:

(a) kuwekeza au anatarajia kuwekeza mtaji wenye thamani usiopungua Dola za Kimarekani Laki Tatu kwa miradi ya hoteli au Dola za Kimarekani Laki Moja kwa miradi mengine; na

(b) kufanya biashara halali kama zilivyowekwa katika Sheria hii.

**3.** Kwa kuzingatia masharti ya aya ya 1 na ya 2 ya Jadweli hili, muombaji:

(a) atawasilisha dhana ya mradi kupitia fomu ya kuonesha nia ya uwekezaji ambayo itapatikana bila ya malipo katika Mamlaka;

(b) baada ya kurejesha fomu ya kuonesha nia ya uwekezaji, Mamlaka italazimika kumjuilisha kuwa anatakiwa achukue Fomu ya Maombi ya Uwekezaji au kushauri vyenginevyo ndani ya siku tatu za kazi;

(c) iwapo ametakiwa kuchukua Fomu ya Maombi ya Uwekezaji, atalazimika kufanya hivyo baada ya kulipa ada ya Dola za Kimarekani Mia Tano katika Mamlaka ambazo hazitarejeshwa,

(d) Baada ya Muombaji kujaza fomu ya maombi ya uwekezaji ipasavyo, atatakiwa kuiwasilisha pamoja na nyaraka zifuatazo katika Mamlaka:

(i) nakala kumi za Mpango wa Biashara au upembuzi yakinifu;

(ii) Hati ya usajili wa kampuni au hati ya kukidhi vigezo ambapo usajili wa kampuni hiyo umefanyika nje ya Zanzibar;

(iii) Katiba na kanuni za kampuni;

(iv) uthibitisho wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi au mradi unaopendekezwa;

(v) nakala za hati ya kusafiria, picha za paspoti na maelezo binafsi ya kila mmiliki wa hisa;

(vi) cheti cha uthibitisho wa tabia njema cha polisi kutoka nchi anayotoka kwa kila mmiliki wa hisa na wakurugenzi wa kampuni;

(vii) ruhusa au leseni kutoka sekta ya mradi aliowekeza au anaotegemea kuwekeza;

(viii) uthibitisho wa malipo ya fomu ya maombi ya mradi; na

(ix) nyaraka nyengine yoyote itakayoweza kusaidia katika maombi.

(e) Kwa kuzingatia aya (d) (i) ya kifungu hiki, upembuzi yakinifu au Mpango wa Biashara utajumuisha angalau yafuatayo:

(i) jina la mradi unaotarajiwa kuwekezwa na taarifa zinazohusiana na biashara yake;

(ii) mpango wa utekelezaji wa mradi na muda unaotarajiwa kuanza;

(iii) uchambuzi wa masoko unaojumuisha taarifa za masoko muhimu, wateja na washindani wake;

(iv) uendeshaji wa biashara unaojumuisha taarifa za kina za malighafi zinazotakiwa na vyanzo vyake, teknolojia itakayotumika, mipango ya kubadilishana ujuzi, fedha na mali ambazo chanzo chake ni kutoka nje ya nchi na muda ambao fedha na mali hizo zitawekezwa, muundo wa taasisi na rasilimali watu inayohitajika kwa mradi unaopendekezwa;

(v) mpango wa fedha wa miaka mitano ambao utaonesha upatikanaji wa fedha, upembuzi wa kina na madhara yanayoweza kutokea kwa Uwekezaji; na

(vi) taarifa za kina au uchambuzi wa kimazingira na mambo ya kijamii.

**4.** Mamlaka ndani ya siku saba za kazi, itafanya uamuzi wa kumpa mwekezaji cheti cha uwekezaji cha mpito au kumshauri vyenginevyo.

**5.** Mwekezaji atalipa ada ya Cheti cha Uwekezaji kama ilivyotajwa katika Sheria na kuainishwa katika Kanuni zilizowekwa chini ya Sheria hii.

**6.** Cheti za Uwekezaji kitatolewa upya kila mwaka mpaka mtaji halisi uliokadiriwa kuwekezwa utakapokamilika.

## JADWELI LA PILI

---

## TARATIBU ZA UTOAJI VIVUTIO KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA IKIJUMUISHA UWEKEZAJI MKAKATI

**[Chini ya kifungu 6(b)]**

---

### SEHEMU YA KWANZA

**Taratibu za Maombi kwa Vivutio vya Kodi ya Mapato ya Kampuni**

**1.** Katika kuhakikisha kwamba wawekezaji wanarejesha gharama za uwekezaji wao kabla ya kulipa kodi ya mapato ya kampuni, Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae amewekeza kiwango kisichopungua asilimia sabini ya tano cha mtaji ulioelezwa katika mpango wake wa biashara au upembuzi yakinifu uliothibitishwa na Mamlaka, na kuanza kufanya shughuli za biashara, anaweza kuomba kwa maandishi kwa Mamlaka msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni na kuambatanisha katika maombi yake nyaraka zifuatazo:

(a) hesabu zilizokaguliwa na kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar;

(b) taarifa ya utekelezaji juu ya uwekezaji uliofanywa;

(c) cheti cha uthibitisho cha mlipa kodi kutoka Mamlaka za kodi; na

(d) leseni halali ya biashara.

**2.** Maombi yatafanywa katika mwaka wa mwanzo wa utekelezaji wa biashara.

### SEHEMU YA PILI

**Utaratibu wa Maombi ya Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani au Ushuru wa Forodha.**

**1.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa atapatiwa kibali cha ujenzi kilichotolewa na mamlaka husika pale ambapo mradi unaopendekezwa unahusiana na ujenzi; mara baada ya kutolewa kibali cha ujenzi, mmiliki wa Cheti cha Uwekezaji atawasilisha cheti chake kwa Mamlaka, nakala nne za makisio ya gharama za ujenzi unaotaka kufanywa na nakala nne za michoro iliyothibitishwa.

**2.** Kwa mradi wa uwekezaji ambao hauhusiani na ujenzi, mmiliki wa Cheti cha Uwekezaji atawasilisha nakala nne za orodha za mashine, zana, malighafi na mahitaji **yoyote** mengine yatakayohitajika katika kuendelea na uwekezaji uliopendekezwa.

**3.** Mamlaka itazingatia makisio ya ujenzi yaliyowasilishwa, michoro na orodha ya vitu na kuvithibitisha kama inavyohitajika, ndani ya siku kumi na nne za kazi; nakala ya orodha ya vitu vilivyothibitishwa atapewa mmiliki wa cheti cha uwekezaji na atakitumia kama ni kumbukumbu kwa maombi yajayo ya msamaha.

**4.** Kwa kuzingatia aya ya 3 ya Jadweli hili, kila mzigo wa bidhaa utakaoingizwa, Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaweza, kuomba kwa Mamlaka msamaha angalau siku kumi na nne za kazi kabla mzigo haujafika Zanzibar; maombi yataambatanishwa na:

(a) nyaraka za kusafirishia mizigo kwa njia ya bahari au anga, taarifa za mzigo au nyaraka za ndani za mauzo;

(b) nyaraka ya utoaji mizigo;

(c) stakabadhi ya mauzo; na

(d) orodha ya vitu vilivyomo.

**5.** Kwa kuzingatia aya ya 3 ya Jadweli hili, kwa ununuzi wowote wa ndani, Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaweza kuomba punguzo la Kodi ya Ongezeko la Thamani; ombi litaambatanishwa na nakala tatu za:

(a) fomu ya kodi ya Ongezeko la Thamani iliyojazwa kikamilifu kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar; na

(b) nakala ya stakabadhi ya bei.

**6.** Mamlaka inaweza, ndani ya siku kumi na nne za kazi, kuthibitisha msamaha au kumshauri muombaji vyenginevyo.

**7.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa atalazimika kulipa kwa Mamlaka asilimia tano ya kiwango kilichosamehewa ikiwa ni ada ya huduma.

## JADWELI LA TATU

## UTARATIBU NA VIGEZO VYA MAOMBI KWA UWEKEZAJI MKAKATI

**[Chini ya kifungu 6(c)]**

## SEHEMU KWANZA

### Utaratibu wa Maombi kwa Uwekezaji Mkakati

**1.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaweza kuomba kwa Mamlaka kupatiwa hadhi kuwa Uwekezaji Mkakati kwa mujibu wa masharti na vigezo vilivyoainishwa katika SEHEMU YA PILI ya Jadweli hili.

**2.** Mamlaka itazingatia ombi na inaweza kupendekeza kwa Waziri kutoa hadhi ya Uwekezaji Mkakati kwa muombaji.

**3.** Waziri, baada ya kushauriana na taasisi husika, atatoa uamuzi wa aidha kukubali au kukataa hadhi ya kuwa Mwekezaji Mkakati na kumjulisha muombaji ipasavyo.

**4.** Waziri anaweza kutengua hadhi ya kuwa Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae amepewa hadhi ya Uwekezaji Mkakati katika mazingira yoyote ikiwa:

(a) atashindwa kutekeleza wajibu aliopewa chini ya Sheria hii;

(b) atashindwa kutimiza vigezo na masharti ya Uwekezaji Mkakati; au

(c) atafanya jambo lolote ambalo limekatazwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU PILI

### Vigezo vya Uwekezaji Mkakati

**1.** Mwekezaji aliyeidhinishwa anaweza kupewa hadhi ya kuwa Mwekezaji Mkakati baada ya:

(a) Kuwekeza mali zenye thamani sawa na Dola za Kimarekeni Milioni Mia Moja au zaidi na kuchangia angalau asilimia thelathini ya uwekezaji huo katika utaratibu ulio sawa;

(b) Kuajiri angalau watu elfu moja; au

(c) Kuwekeza mali zenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni Hamsini katika Uwekezaji wa ubunifu au katika maeneo yaliyopungukiwa na fursa za kiuchumi katika sekta zifuatazo zilizopewa kipaumble:

(i) Uzalishaji wa viwandani au uunganishaji;

(ii) Masoko makubwa ya utalii;

(iii) Kilimo na uvuvi;

(iv) Uendelezaji wa majengo;

(v) Nishati;

(vi) Uendelezaji miundombinu; na

(vii) Teknolojia ya habari na mawasiliano.

## JADWELI LA NNE

---

## BIASHARA ZILIZOTENGWA KWA WAZANZIBARI

**[Chini ya kifungu cha 20(3)]**

---

**1.** Biashara ambazo zimetengwa kufanywa na Wazanzibari pekee ni:

(a) Duka la vinyozi, ususi na vipodozi;

(b) duka la biashara za jumla na reja reja;

(c) mwendeshaji wa shughuli za kitalii;

(d) mgahawa (isipokuwa mikahawa maalum);

(e) nyumba ya kulala wageni;

(f) wakala wa usafirishaji;

(g) ukulima mdogo;

(h) duka la zawadi;

(i) huduma za usafi wa nyumba au Ofisi;

(j) huduma ya ulinzi wa nyumba au Ofisi;

(k) duka la 'ice - cream';

(l) Duka la vinywaji na vileo;

(m) Huduma za usambazaji bidhaa na vifaa; na

(n) uvuvi mdogo.

**2.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha kwanza cha jadweli hili, biashara zote ambazo mtaji wake utakuwa chini ya Dola za Kimarekani Laki Tatu hazitoruhusiwa kufanywa na wawekezaji wa kigeni.

## JADWELI LA TANO

## YANAYOTAKIWA KUWEMO KATIKA CHETI CHA UWEKEZAJI

**[Chini ya kifungu cha 24]**

Cheti cha Uwekezaji kinachotolewa chini ya kifungu cha 23(3) cha Sheria hii kitajumuisha:

(a) jina la biashara;

(b) jina la mradi wa uwekezaji uliowekezwa au unaotarajiwa kuwekezwa;

(c) shughuli zinazotegemewa kufanywa;

(d) sekta ya uchumi iliyowekezwa au inayotegemewa kuwekezwa;

(e) eneo la mradi wa uwekezaji lililowekezwa au linalotegemewa kuwekezwa;

(f) kiwango cha mali kilichowekezwa au kinachotegemewa kuwekezwa;

(g) taarifa inayohusiana na muda ambao mtaji utakuwa umewekezwa;

(h) taarifa itakayohusiana na aina ya Uwekezaji utakaotekelezwa;

(i) taarifa zinazomruhusu mwekezaji kutekeleza uwekezaji wake;

(j) aina ya cheti kilichotolewa;

(k) taarifa zinazoonesha tarehe ya Cheti cha Uwekezaji kilipotolewa;

(l) taarifa zinazoonesha uhalali wa Cheti cha Uwekezaji; na

(m) jambo jengine lolote ambalo ni muhimu au linalohitajika kwa madhumuni ya Sheria hii.

## JADWELI LA SITA

---

## FURSA, VIVUTIO NA MSAMAHA KWA UWEKEZAJI MKAKATI

**[Chini ya kifungu cha 31(2)]**

---

## SEHEMU YA KWANZA

**Fursa, Vivutio na Ruhusa wakati wa Utekelezaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.**

**1.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae amepewa hadhi ya kuwa Mwekezaji Mkakati, anaweza kupatiwa fursa, vivutio na ruhusa zifuatazo wakati wa uendelezwaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa kadri inavyohitajika:

(a) msamaha wa ushuru na kodi zote wa uingizaji na ununuzi wa ndani wa vifaa na bidhaa za ujenzi wakati wa ujenzi wa miradi;

(b) msamaha wa kodi ya mapato wa kipindi cha miaka mitano kwa riba ya mkopo wa mtaji uliokopwa kutoka benki za kigeni;

(c) msamaha wa kodi ya ardhi kwa miaka mitano;

(d) umiliki wa kigeni wa asilimia mia unaruhusiwa;

(e) kutumia wakandarasi wa kigeni inaruhusiwa; na

(f) msamaha wa kodi ya baharini kwa miaka mitano kwa miradi ya utalii.

## SEHEMU YA PILI

**Fursa, Vivutio na Ruhusa wakati wa Uendeshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.**

**2.** Mwekezaji aliyeidhinishwa ambae amepewa hadhi ya kuwa Mwekezaji Mkakati, anaweza kupatiwa fursa, vivutio na ruhusa zifuatazo wakati wa uendeshwaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa kadri inavyohitajika:

(a) msamaha wa asilimia hamsini ya kodi ya mapato inayopaswa kulipwa na kampuni;

(b) msamaha wa asilimia hamsini wa aida inayotakiwa kuhamishwa;

(c) msamaha wa asilimia hamsini ya kodi inayotokana na uchakavu wa vitu kwa miaka mitano;

(d) msamaha wa kodi ya mapato wa kipindi cha miaka mitano kwa riba ya mkopo wa mtaji uliokopwa kutoka benki za kigeni;

(e) msamaha wa asilimia mia moja katika kazi za utafiti na maendeleo;

(f) ruhusa ya kubakiza asilimia mia ya faida baada ya malipo ya kodi; na

(g) umiliki wa kigeni unaruhusiwa kwa asilimia mia.

**3.** Bila ya kuathiri aya ya 1 na ya 2 ya Sehemu hii, Uwekezaji Mkakati katika sekta ya uzalishaji, anaweza kupatiwa vivutio vifuatavyo vya ziada:

(a) msamaha wa kulipa kodi yoyote kwa bidhaa zote zinazozalishwa kwa kusafirishwa nje ya nchi;

(b) msamaha wa kulipa ushuru wa biashara kwa malighafi zote na pembejeo za viwanda zinazonunuliwa kutoka Tanzania Bara;

(c) msamaha wa kulipa ushuru wa uingizaji, ushuru wa bidhaa na kodi ya ongezeko la thamani katika ununuzi wa bidhaa za ndani za mashine nzito au vifaa vinavyohitajika wakati wa uzalishaji;

(d) msamaha wa kulipa kodi ya ongezeko la thamani katika ununuzi wa bidhaa za ndani za mashine nzito au vifaa vinavyohitajika wakati wa uzalishaji; na

(e) ziada ya miaka mitano ya ruhusa ya asilimia hamsini ya kodi inayotokana na uchakavu wa vitu.

JADWELI LA SABA

---

# VIVUTIO NA RUHUSA KWA MWEKEZAJI ALIYEIDHINISHWA

**[Chini ya kifungu cha 31(3)]**

---

## SEHEMU YA KWANZA

### Vivutio na Ruhusa katika Maeneo Huru ya Uchumi

### KUNDI "A": WAENDELEZAJI MAENEO HURU YA UCHUMI: MAENDELEO YA MIUNDOMBINU

**1.** Muendelezaji wa Maeneo Huru ya Uchumi atafaidika kwa vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha kutokana na malipo ya kodi na ushuru kwa mashine, zana, gari za kazi nzito, majengo, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyengine zozote zilizo na sifa ya mtaji ambazo zitatumika kwa madhumini ya uendelezaji wa miundombinu ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(b) msamaha kutokana na malipo ya ushuru wa mapato ya kampuni kwa kipindi cha mwanzo cha miaka kumi, na baadae ushuru wa mapato ya kampuni utatozwa kwa kiwango kilichofafanuliwa katika Sheria ya Kodi ya Mapato;

(c) msamaha kutokana na malipo ya kodi ya zuio inayotokana na pango, gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(d) msamaha kutokana na malipo ya kodi ya mali kwa miaka kumi ya mwanzo;

(e) punguzo la ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyengine yoyote inayotolewa kwa ajili ya uingizaji nchini wa gari moja ya utawala, gari la kubebea wagonjwa, gari na zana za kuzimia moto na gari mbili kwa ajili ya kuwapeleka na kurejesha wafanyakazi katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(f) msamaha kutokana na malipo ya ushuru wa stempu kwa hati yoyote inayotekelezwa ndani au nje ya Maeneo Huru ya Uchumi inayohusiana na uhaulishaji, ukodishaji au dhamana ya mali yoyote inayohamishika

au isiohamishika iliyomo ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi au nyaraka yoyote, cheti, hati, ripoti, taarifa au kumbukumbu inayohusiana na shughuli yoyote, kitendo, uendeshaji, mradi, utekelezaji, uwekezaji ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(g) msamaha kutokana na ukaguzi kabla ya kusafirisha au baada ya kuingia; na

(h) ukaguzi wa bidhaa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi.

## KUNDI "B" WAENDESHAJI MAENEO HURU YA UCHUMI: WAWEKEZAJI WALIOIDHINISHWA WANAOZALISHA KWA AJILI YA KUUZA NDANI YA ENEO LA UDHIBITI WA FORODHA

**1.** Wawekezaji walioidhinishwa ambao mauzo yao yanafanyika ndani ya eneo la Udhibiti wa Forodha watastahiki:

(a) punguzo la ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na tozo lolote la ushuru kwa mali ghafi na bidhaa za mtaji zinazohusiana na uzalishaji katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(b) msamaha kutokana na malipo ya kodi la zuio kwa riba ya mkopo wa kigeni;

(c) punguzo la ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyengine yoyote inayotolewa kwa ajili ya uingizaji nchini wa gari moja ya utawala, gari la kubebea wagonjwa, gari na zana za kuzimia moto na gari mbili kwa ajili ya kuwapeleka na kurejesha wafanyakazi katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(d) msamaha kutokana na ukaguzi kabla ya kusafirisha au baada ya kuingia;

(e) ukaguzi wa bidhaa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(f) kupata huduma zenye ushindani, za kisasa na za uhakika zinazopatikana ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi; na

(g) kwa kuzingatia masharti na utaratibu wa ubadilishaji fedha za kigeni na ulipaji kodi kwa kadiri itakavyokuwa, kuhaulisha fedha inayobadilishika bila ya masharti kupitia wakala wa benki yeyote aliyeidhinishwa kwa:

(i) faida inayopatikana au gawio lililotokana na uwekezaji;

(ii) malipo yanayohusiana na huduma za mkopo iwapo mkopo kutoka nje umepatikana;

(iii) mrabaha, ada na tozo zinazohusiana na makubaliano ya ubadilishanaji wa teknolojia;

(iv) kutuma fedha zinazotokana na faida ya biashara au riba inayotokana na biashara yoyote iliyoruhusiwa; na

(v) malipo ya mishahara na mafao mengine kwa wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa Tanzania kwenye biashara iliyoruhusiwa.

## KUNDI "C" WAENDESHAJI MAENEO HURU YA UCHUMI: WAWEKEZAJI WALIOIDHINISHWA WANAOZALISHA KWA AJILI YA KUUZA KATIKA MASOKO YA NJE

**1.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa anaezalisha kwa ajili ya soko la nje katika eneo ambalo si la viwanda au sekta ya uchakataji atastahiki:

(a) kwa kuzingatia vigezo na utaratibu, kupata dhamana ya mkopo wa usafirishaji nje;

(b) punguzo la ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyengine zinazotolewa kwa malighafi kwa bidhaa zinazotokana na mtaji kwa uzalishaji katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(c) msamaha kutokana na malipo ya ushuru wa mapato ya kampuni kwa kipindi cha mwanzo cha miaka kumi, na baadae ushuru wa mapato ya kampuni utatozwa kwa kiwango kilichofafanuliwa katika Sheria ya Kodi ya Mapato;

(d) msamaha kutokana na malipo ya kodi ya zuio inayotokana na ukodishaji, gawiyo na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(e) msamaha kutokana na malipo ya ushuru na kodi zote zinazotozwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika Maeneo Huru ya Uchumi kwa kipindi cha miaka kumi;

(f) msamaha kutokana na ukaguzi kabla ya kusafirisha au baada ya kuingia;

(g) ukaguzi wa bidhaa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi;

(h) punguzo la ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyengine yoyote inayotolewa kwa ajili ya uingizaji nchini wa gari moja ya utawala, gari la kubebea wagonjwa, gari na zana za kuzimia moto na gari mbili kwa ajili ya kuwapeleka na kurejesha wafanyakazi katika Maeneo Huru ya Uchumi;

(i) ushughulikiaji wa bidhaa zilizoingizwa ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi kama bidhaa za mpito;

(j) kupata huduma zenye ushindani, za kisasa na za uhakika zinazopatikana ndani ya Maeneo Huru ya Uchumi; na

(k) kwa kuzingatia masharti na utaratibu wa ubadilishaji fedha za kigeni na ulipaji kodi kwa kadiri itakavyokuwa, kuhaulisha fedha inayobadilishika bila ya masharti kupitia wakala wa benki yeyote aliyeidhinishwa kwa:

(i) faida inayopatikana au gawio lililotokana na uwekezaji;

(ii) malipo yanayohusiana na huduma za mkopo iwapo mkopo kutoka nje umepatikana;

(iii) mrabaha, ada na tozo zinazohusiana na makubaliano ya ubadilishanaji wa teknolojia;

(iv) kutuma fedha zinazotokana na faida ya biashara au riba inayotokana na biashara yoyote iliyoruhusiwa;

(v) malipo ya mishahara na mafao mengine kwa wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa Tanzania kwenye biashara iliyoruhusiwa;

(l) asilimia ishirini ya uzalishaji anaruhusiwa kuuza katika soko la ndani na atawajibika kulipa kodi zote;

(m) asilimia mia moja ya umiliki wa mgeni unaruhusiwa; na

(n) hakuna kikomo cha muda wa bidhaa zilizohifadhiwa katika Maeneo Huru ya Uchumi.

**2.** Kwa madhumini ya kifungu hiki, wawekezaji wenye leseni iliotolewa maalumu kwa soko la nje ni wawekezaji ambao uzalishaji wao wa mwaka kwa zaidi ya asilimia themanini unasafirishwa nje.

## SEHEMU YA PILI

### Fursa na vivutio nje ya Maeneo Huru ya Uchumi

**1.** Mwekezaji Aliyeidhinishwa anayewekeza nje ya Maeneo Huru ya Uchumi anaweza kupatiwa:

(a) msamaha kutokana na kodi ya uingizaji, ushuru wa bidhaa, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyenginezo kwa mashine, vifaa, vipuri, malighafi, gari na bidhaa nyengine ambazo ni muhimu na ambazo ni maalum kwa ajili ya mradi wakati wa ujenzi kama ilivyooneshwa katika Cheti cha Uwekezaji;

(b) msamaha kutokana na ada ya leseni ya biashara kwa miezi mitatu ya mwanzo ya majaribio ya mradi;

(c) msamaha wa kodi ya kampuni kwa miaka mitano;

(d) umiliki wa mgeni kwa asilimia mia moja;

(e) zuio la faida kwa asilimia mia moja baada ya kulipa kodi;

(f) ruhusa ya asilimia mia moja katika utafiti na maendeleo; na

(g) ruhusa ya kuhaulisha faida kwa asilimia mia moja baada ya kodi.

**2.** Bila ya kuathiri masharti ya aya ya 1 ya sehemu hii, Mwekezaji Aliyeidhinishwa anayewekeza katika sekta ya utengenezaji anaweza pia kupatiwa:

(a) msamaha kutokana na malipo ya kodi yoyote ya bidhaa zilizozalishwa kwa ajili ya usafirishaji wa nje;

(b) msamaha kutokana na malipo ya kodi za biashara kwa ajili ya malighafi na bidhaa za viwandani zilizonunuliwa Tanzania bara;

(c) msamaha kutokana na malipo ya kodi ya uingizaji, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyengine zinazolingana na hizo, malighafi na vifungashio wakati wa uendeshaji wa mradi;

(d) msamaha wa kodi ya mapato katika riba inayotokana na mtaji uliokopwa uliosajiliwa; na

(e) asilimia mia moja ya punguzo la mtaji uliotumika ndani ya miaka mitano.

3. Bila ya kuathiri masharti ya aya ya 1 ya Sehemu hii, Mwekezaji Aliyeidhinishwa ambae amewekeza katika biashara ya majengo anaweza pia kupewa:

(a) msamaha wa kodi ya mapato katika riba inayotokana na mtaji uliokopwa;

(b) msamaha wa ushuru wa stempu;

(c) asilimia mia moja ya punguzo la mtaji uliotumika ndani ya miaka mitano; na

(d) msamaha wa kodi la ongezeko la mtaji kwa mali zilizouzwa au kununuliwa.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tarehe 30 Novemba, 2018.

..............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***

***Zanzibar.***